



Maswali Na majibu

Q. Madharau ni nini?

Hii ni njia ya kubainisha watu , na kuwatofautisha na watu wengine , hii ni kudharau watu wenye virusi vya ukimwi.

Q. Watu wenye virusi vya ukimwi hudharauliwa aje?

Watu wenye virusi vya ukimwi hudharauliwa na watu wengi katika jamaa.Hii hufanyika kwa njia mingi kama vile kunyimwa kazi na pia kukosa matibabu , watoto pia hutupwa na pia huumia sana kama wana virusi au kama wazazi wao wana virusi kwani hudharauliwa, kwa mfano kuna watoto ambao hutupwiwa mawe kwasababu wazazi wao wameaga dunia kwa sababau ya ugonjwa wa ukimwi.

Q. Kuna madharau aina gani?

Watu wengi amabao hawana virusi huogopa , huona haya na pia hukataa na kudharau wale wana virusi vya ukimwi.

Q. Kwanini watu wenye virusi vya ukimwi hudharauliwa?

Ugonjwa huu ni hatari na hii hufanya watu wengi kuogopa ugonjwa huu; Pili njia moja ya kueneza ugonjwa huu ni kwa kufanya mapenzi na watu wengi huona haya na hawataki kuongea juu ya kufanya mapenzi.

Q. Hii inajalisha?

Ndio , Madharau ni njia moja ambayo inazuia watu kuongea juu ya ugonjwa wa ukimwi.Wakati watu wanadharauliwa wanaona hakuna haja ya kuenda hospitali kupata matibabu, Kama jamii inadharau watu wenye virusi basi inaweka vikwazo kwa watu hawa na wengi wao wanakataa ya kwamba wana virusi hii na kwa hivyo watu hawabadilishi tabia zao na kwa hivyo nambari ya watu wenye virusi inaendelea kuongezeka na inazuia masomo kuhusu ugonjwa huu.

Q. Tukiweka watu wenye virusi kando na wale hawana , hii itateremsha nambari ya watu wenye virusi?

Hapana, hii itasababisha madharau na hakuna mtu yeyote ataenda kupimwa kwani wanaogopa kudharauliwa.Na hii itamaanisha nambari ya watu wenye virusi itaongezeka kwani hakuna mtu atajua ali yake